

## SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)



### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU SUMUKUVU AINA YA PATULIN KWENYE JUISI YA TUFAA (APPLE) AINA YA CERES

**Dar es Salaam, 16 Oktoba, 2021**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kuutaarifu umma kuwa hivi karibuni lilipokea taarifa kutoka mtandao wa Kimataifa wa Mamlaka za Udhhibiti Usalama wa Chakula (***International Food Safety Authorities Network (INFOSAN)***) uliopo chini ya *FAO* na *WHO* kuhusu uwepo wa sumukuvu aina ya Patulin kwenye juisi ya tufaa (apple) aina ya Ceres kwenye **matoleo ya tarehe 14 hadi 30 Juni, 2021.**

Patulin ni sumu inayotokana na kuvu aina ya *Aspergillus*, *Penicillium* na *Byssochlamys* ambao huzalisha sumu ikiwa matunda ya tufaa (apples) yatakuwa yameanza kuoza. Madhara ya patulin ni kuchafuka tumbo, kichefuchefu na kutapika.

Mara baada ya kupata taarifa hizo kutoka kwenye mtandao huo wa INFOSAN, tulichukua hatua zifuatazo:

- 1) Kufuatilia taarifa za uwepo wa matoleo hayo ya juisi za tufaa ya tangu tarehe 14 hadi 30 Juni, 2021;
- 2) Kumtembelea wakala wa msindikaji (*sole distributor*) aliyepo Dar-es-Salaam na kukagua nyaraka za juisi zilizolingizwa kipindi cha nyuma na juisi zilizopo kwenye ghala.

Baada ya ufuatiliaji huo wa kina TBS ilibaini kuwa matoleo ya juisi za tufaa (apple ceres juice) ya mwezi Juni, 2021 **HAYAJAINGIA NCHINI** na tutaendelea kuhakikisha hayatoingia nchini.

Aidha, tunapenda kuutaarifu umma wa Tanzania kuwa mabadiliko ya sheria (Sheria ya Fedha Na. 8 ya mwaka 2019) ya kuhamisha majukumu ya kudhibiti usalama wa chakula na vipodozi kutoka iliyokuwa TFDA na kuja TBS hayajaathiri udhibiti wa bidhaa hizo nchini kwa kuwa hakuna kazi ya udhibiti ambayo ilifanyika na TFDA ambayo haifanyiki TBS ikiwemo:

- 1) Usajili wa majengo na bidhaa kwa wazalishaji wa ndani unaendelea kupitia mifumo ya uthibiti ubora iliyopo ambapo matakwa ya usajili yaliyokuwa yakizingatiwa na TFDA yameingizwa;
- 2) Usajili wa bidhaa kutoka nje ya nchi unaendelea kufanyika kama ulivyokuwa unafanyika awali na TFDA; na
- 3) Ufuatiliaji wa vihatarishi (*Food Risk Assessment*) unaendelea kufanyika kama ilivyokuwa awali wakati wa TFDA.

Tunapenda kuuhakikishia umma kuwa tunaendelea kulinda usalama na ubora wa bidhaa zote wakati wote.

Kwa maelezo zaidi tafadhali piga namba ya bure: 0800110827

Imetolewa na:



Gladness H. Kaseka

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Masoko